JARIDA LA MTANDAONI www.owm.go.tz JUNE 2025

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU



## WAZIRI MKUU: Tanzania siyo mahali salama kwa biashara ya dawa za kulevyya

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.





WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa ametoa onyo kwa wasambazaji na wauzaji wa dawa za kulevya kwamba Tanzania siyo mahali pa kufanyia biashara zao.

Waziri Mkuu ambaye amefunga maadhimisho ya Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani kwa niaba ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema: "Tanzania siyo mahali salama kwa wauzaji, wasafirishaji na walimaji na hata pia watumiaji wa dawa za kulevya. Tanzania tumeiva na sasa tunaenda kukomesha biashara hii."

Ametoa kauli hiyo leo jioni wakati akizungumza na maelfu ya wakazi wa dodoma wakiwemo wananchi, wadau, viongozi wa serikali, wa dini na siasa ambao walihudhuria kilele cha maadhimisho hayo kwenye ukumbi wa mikutano wa jakaya kikwete, jijini dodoma.

"Makamishna na wakuu wa vyombo vya ulinzi fanyeni kazi, imarisheni ulinzi iwe ni kwenye SGR, vituo vya mabasi, bandari na viwanja vya ndege ili tuweze kuokoa vijana wetu. Dawa hizi zina madhara makubwa kwani zinapoteza uwezo wa mwili na uwezo wa kiakili wa kufikiri mambo," amesisitiza.

Amesema kuwa anatambua kwamba kuna mjadala ulioibuka baina ya wachumi na wadau wa kuzuia matumizi ya dawa za kulevya huku wachumi wakidai kuwa zinaleta fedha na kuacha kuangalia madhara ya kiafya ambayo wadau wanayasemea. "Kama tunataka tuwe na kundi la vijana wa Kitanzania mazezeta, basi turuhusu hii biashara. Lakini, Serikali hii tumekataa kwa sababu tunaamini kuwa hiyo mijadala haina tija na hatutairuhusu," amesisitiza Waziri

Amesema kazi kubwa ya uwekezaji kwenye eneo hilo imefanywa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ameongeza bajeti ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA) na kuwapatia vyombo vya usafiri ili wafanye kazi yao kwa ufanisi zaidi.

Akielezea kuhusu ugumu uliokuwepo wa kuhitimisha kesi za watu waliokuwa wanakutwa na dawa hizo, Waziri Mkuu amesema: "Lazima tulipongeze Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuruhusu Sheria ya Dawa za Kulevya itungwe; na hii ilikuwa ni baada ya kubaini kulikuwa na mapungufu kwenye mfumo wetu wa sheria," amesema.

Aliwaeleza washiriki wa maadhimisho hayo kwamba kutokana na uwepo wa sheria hiyo, katika kila kesi 100 zinazofikishwa mahakamani, Serikali imeweza kushinda kesi 76.

Amesema ufanisi mkubwa unaoonekana hivi sasa unatokana na kufungamanishwa kwa Mamlaka ya DCEA ya Tanzania Bara na ile ya ZDCEA ya Zanzibar ambazo zinafanya kazi kwa karibu. "Kwa hiyo

Mapema, akimkaribisha Waziri Mkuu kuzungumza na washiriki hao, Naibu Waziri wa Nchi (OWM – Sera, Bunge na Uratibu) Ummy Nderianga alisema Rais Samia ameweka fedha nyingi na vifaa ili kuhakikisha anawaokoa vijana wa Kitanzania kutoka kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

Amesema Ofisi ya Waziri Mkuu imeongeza operesheni na usimamizi kwa kufungua ofisi za kanda ambapo mkoa wa Dodoma tayari unayo ofisi ya Kanda.




# Waziri Lukuvi Aitaka Bodi ya ATF Kufikia Malengo Kutokomeza UKIMWI 2030

Serikali inategemea Bodi ya Mpya ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI italeta fikra mpya, mbinu mpya, na weledi wa hali ya juu ili kuhakikisha Mfuko huo unakuwa chombo madhubuti cha kuhakikisha Tanzania inafikia malengo yake ya kutokomeza UKIMWI ifikapo Mwaka 2030.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu Mhe. William Lukuvi (MB) wakati akizinduza Bodi ya Tatu ya Mfuko wa Udhamini wa Kudhibiti UKIMWI (AIDS Trust Fund - ATF) leo jijini Dodoma.

Waziri Lukuvi ameeleza kuwa, Bodi hiyo inapaswa kutambua kuwa dunia ipo katika hatua mpya na muhimu ya kimkakati katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI ambapo Tanzania kama sehemu ya jumuiya ya kimataifa imesaini na inatekeleza ahadi na makubaliano mbalimbali ya kimataifa na kikanda.

"Tumejidhatiti kutekeleza Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030), hasa lengo la tatu linalohusu kuhakikisha afya njema na ustawi kwa wote, vilevile, tunaitekeleza kwa dhati Ajenda ya Umoja wa Afrika ya 2063, pamoja na Azimio la Kisiasa la Umoja wa Mataifa la mwaka 2021 kuhusu UKIMWI" amefafanua Waziri Lukuvi.

Aidha, Mhe Lukuvi ameitaka Bodi hiyo kutambua kwamba kwa sasa dunia inashuhudia mabadiliko makubwa katika namna ya kufadhili mapambano dhidi ya UKIMWI.

"Wahisani wakuu wa Kimataifa kama PEPFAR na Global Fund wameshaanza kupunguza kwa awamu michango yao huku wakisisitiza umuhimu wa nchi kuchukua umiliki wa ndani na kuhakikisha uendelevu wa kifedha kwa juhudi zake. Mwelekeo huu unatutaka sisi kama Taifa kuongeza uwezo wetu wa ndani wa kifedha ili kuhakikisha mwitikio wa VVU na UKIMWI unaendelea kwa nguvu, kasi, na mafanikio makubwa".

"Katika muktadha huu, Mfuko wa Udhamini wa UKIMWI (ATF) ni nyenzo muhimu sana katika kuhakikisha Taifa linakuwa na uhakika wa kifedha na usalama wa afya ya wananchi wake" amebainisha Waziri Lukuvi.

Vilevile ameeleza kuwa, Mfuko huo ni alama ya dhamira ya kweli ya Serikali kuhakikisha kuwa huduma za VVU na UKIMWI zinadumu, hata katika mazingira ambapo michango ya wahisani inapungua.

"Kupitia Mfuko huu, tunasisitiza umiliki wa kitaifa ambapo Serikali, sekta binafsi, asasi za kiraia, taasisi za dini, vijana, watu wanaoishi na VVU na jamii kwa ujumla wanashiriki kikamilifu katika juhudi hizi. Mfuko huu pia unaleta msukumo mkubwa wa uwajibikaji wa kisera na kifedha kwa kuhakikisha matumizi ya fedha yanazingatia uwazi na matokeo yanayoonekana" ameongeza.

Akimkaribisha mgeni rasmi, Naibu Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu Bw. Dkt. James Kilabuko kwa niaba ya Katibu Mkuu wa ofisi hiyo Dkt. Jim Yonazi amesema kuwa, "mfuko huu ni jitihada za kujenga misingi imara ya uendelevu wa kifedha wa mapambano dhidi ya UKIMWI ambayo kwa muda mrefu yamekuwa yakitegemea zaidi wahisani kutoka nje, tukio hili linaakisi dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ya kuhakikisha kuwa uendelevu wa mwitikio wa UKIMWI unajengeka kwa msingi wa uhimilivu wa ndani na ushirikiano mpana wa wadau wote wa maendeleo yaa taifa letu".

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi hiyo Sabasaba Mushingi amemshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumuamini na kumchagua yeye kuwa Mwenyekiti pamoja na wajumbe wake na hivyo kuahidi kuisimamia na kuingoza bodi hiyo ili kuweza kutimiza malengo ya majukumu waliyopewa.

.


TRUST
TANZANIA
TACAIDS
MAJUKUMU
Sera na Mkakati wa UKIMWI

# “Ushiriki wa Tanzania Jukwaa la dunia waongeza fursa za kimataifa kukabiliana na maafa” Dk. Yonazi






TANZANIA imeshiriki Jukwaa la Nane la Dunia la Kupunguza Madhara ya Maafa lenye jukumu muhimu katika kuhamasisha na kukuza ushirikiano kati ya Serikali, Wadau na Mfumo wa Umoja wa Mataifa ili kuharakisha utekelezaji wa hatua za kupunguza madhara ya maafa.

Akizungumza wakati wa Mkutano huyo unaoendelea Mjini Geneva Uswisi kuanzia tarehe 02 hadi 6 Juni 2025, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri, Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu Dkt.Jim Yonazi alisema jukwaa hilo ni chombo cha kutathmini, kujadili maendeleo ya utekelezaji na kuimarisha masuala ya usimamizi wa maafa kimataifa kupitia makubaliano ya hiyari ya nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa ambayo yameridhiwa na Makubaliano ya hiyari ya kimataifa yanayotekelezwa kwa sasa ni Mkakati wa Sendai wa Kupunguza Madhara ya Maafa 2015 – 2030

“Jukwaa hili hutumika kama chombo muhimu cha kukuza ushirikiano katika utekelezaji wa ajenda nyingine za kimataifa zinazochangia kupunguza madhara ya maafa, ikiwa ni pamoja na mkataba wa Paris kuhusu mabadiliko ya tabianchi na malengo ya maendeleo endelevu.

Aliongeza kuwa, Matokeo ya jukwaa hilo yanatumika katika kutoa muelekeo wa masuala ya usimamizi wa maafa katika maazimio ya Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, baraza la umoja wa mataifa la kiuchumi na kijamii na jukwaa kuu la kisiasa la umoja wa mataifa kuhusu maendeleo endelevu.

Kwa mujibu wa Dkt. Yonazi ameelezwa kuwa, ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupunguza Madhara ya Maafa imepewa jukumu la kuandaa Jukwaa la Dunia na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Jukwaa hufanyika kila baada ya miaka miwili ambapo tangu mwaka 2007, limefanyika mara saba.

Vilevile alisema jukwaa hilo limejumuisha ajenda kuhusu kuimarisha utekelezaji wa mkakati wa Sendai kwa kuzingatia maendeleo na changamoto zilizoainishwa katika mapitio yake ya muda wa kati na Azimio lake kupitia Baraza la Umoja wa Mataifa 2023,

Ajenda nyingine ilihusu kuimarisha mikakati ya kitaifa na serikali za mitaa na mipango ya kupunguza madhara ya maafa, kwa kuzingatia athari za maafa ya hivi karibuni;

“Jukwaa limejadili namna ya kuimarisha mitandao iliyopo na kuanzisha ushirikiano mpya katika ngazi za kimataifa, kitaifa na wadau wa ndani, kubadilishana ujuzi, teknolojia na uzoefu kuhusu sera, programu na uwekezaji kuhusu kupunguza hatari ya maafa.

Dk.Yonazi alisema matokeo ya ushiriki wa jukwaa hilo ni kuimarisha utekelezaji wa Mkakati wa Sendai kupitia Sheria na Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Maafa kwa kupata uzoefu na fursa za kimataifa na wadau.




# Elimu Kuhusu OWM Sera, Bunge na Uratibu Kuendelea Kutolewa

Mkurugenzi wa Idara ya Uwezeshaji Kiuchumi na Maendeleo ya Sekta Binafsi Bw. Conrad Milinga amesema, maonesho ya Wiki ya Utumishi wa Umma yamewezesha Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kutoa elimu juu ya fursa mbalimbali za kiuchumi kupitia mikopo na mifuko ambayo iko katika sekta mbalimbali zinazohusiana na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

Mkurugenzi Milinga ametoa kauli hiyo wakati wa kilele cha Maadhimisho Wiki ya Utumishi wa Umma yaliyofanyika katika viwanja vya Chinangali park Jijini Dodoma
.

Ameeleza, Ofisi ya waziri Mkuu imetumia maadhimisho ya wiki hiyo kueleza wananchi na wadau mbalimbali kuhusu huduma mbalimbali zinazotolewa na ofisi hiyo ikiwemo Uwezeshaji wananchi kiuchumi, namba ya kujinginga na maafa na alama za taifa ambazo ni Wimbo wa Taifa, Ngao ya Taifa na Bendera ya Taifa.

"Tumeweza kuelimisha wananchi kuhusu mfumo unaotumiwa na Idara ya Menejimenti ya Maafa unaoweza kutambua majanga mapema kabla hayajatoke ili kuwapa wananchi tahadhari ya kujiandaa kabla hayo majanga hayajatokea, tumetoa uelewa kwa wananchi kuweza kufahamu maatumizi sahihihi ya alama za taifa ikiwemo ngao sahihi ya taifa , beti za wimbo wa Taifa ambapo wimbo huo unatakiwa kuimbwa beti zote mbili na rangi sahihi za Bendera ya Taifa", amebainisha Bw. Milinga

Aidha, ameongeza kuwa , ofisi imeweza kutoa elimu kwa umma kuhusu Idara ya Ufutiliaji na Tathimini ya shughuli za serikali inavyohusika katika kutoa taarifa za utekelezaji wa miradi mabalimbali inayotekelezwa hapa nchini.

Mbali na hayo, Mkurugenzi Milinga ametoa wito kwa wananchi kujitokeza katika Maonesho ya Kimataifa ya Sababa ambapo Ofisi ya Waziri Mkuu itashiriki maonesho hayo yanayotarajiwa kuanza tarehe 28 Juni, 2025 Jijini Dar Es Salaam.

"Katika maonesho hayo Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na taasisi zetu zote itanatarajia kushiriki hivyo niwasihi wananchi kutembelea maonesho hayo ili kuweza kupata elimu kuhusu shughuli zote zinazofanya na Ofisi ya Waziri Mkuu.



Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na
kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



Tanzania imeshiriki maadhimisho ya miaka 25 ya Jumuiya ya Tathimini Afrika (AFrEA) yanayofanyika kwa siku tatu kuanzia tarehe 16 hadi 18 Juni, 2025 katika kituo cha Mikutano cha Umoja wa Mataifa (UNECA) Jijini Addis Ababa Ethiopia.

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480